



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: 0232935443  
Nukushi: 0232935442  
Barua pepe: [td@nanyambatc.go.tz](mailto:td@nanyambatc.go.tz)

2 BARABARA YA BOMANI,  
S.L.P 1490,  
63682 NANYAMBA-MTWARA

Tarehe : 06/08/2023

**TANGAZO LA KUPATA WAZABUNI WA VIFAA VYA UJENZI  
KATIKA HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA**

Halmashauri ya Mji Nanyamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imepokea fedha kutoka kwa wafadhili wanaoitwa GPE-LANES kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa mawili ya Awali ya Mfano na Ujenzi wa matundu 6 ya vyoo katika shule ya msingi Namkuku. Mradi huu umepata Msamaha wa kodi hivyo bidhaa za ujenzi zitakazotumika katika ujenzi wa shule ya msingi Namkuku hazitajumuisha kodi. Hivyo inatangazwa zabuni ya kuwapata wasambazaji wa vifaa vya ujenzi lakini vyenye msamaha wa kodi.

Baadhi ya vifaa vya ujenzi vinavyohitajika ni kama ifuatavyo kwa kuzingatia msamaha wa kodi.

Na.	JINA LA KIFAA
1	Nondo misumari na wire Mesh
2	Mbao
3	Vifaa vya dari (gypsum boards,Pvc etc)
4	Rangi na Vifaa vya Umaliziaji
5	Marumaru
6	Mabati, Kofia na Misumari ya Bati
7	Vifaa vya Umeme na Maji
8	Saruji

Hivyo, **Mkurugenzi wa Mji Nanyamba** anawatangazia wananchi, Wazabuni na Wasambazaji wa vifaa/bidhaa wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kusambaza vifaa vya ujenzi ambavyo vitatumika kujenga Majengo yaliyoainishwa hapo juu.

Sifa na masharti kwa wananchi, wasambazaji na wazabuni wanaohitajika ni kama ifuatavyo: -

- 1) Muombaji lazima awe na Leseni ya biashara ya bidhaa husika na awasilishe nyaraka zifuatazo:
  - a) Nakala ya Leseni ya Biashara
  - b) Cheti cha Namba ya Utambulisho ya Mlipa kodi (TIN)
  - c) Cheti cha usajili wa "BRELA"
  - d) Barua inayoonesha kwamba bei ya vifaa vya ujenzi alivyojaza hazitabadilika kwa muda wa miezi sita (06)
  - e) Barua ya maombi ikitaja vifaa vya ujenzi anavyoomba
  - f) Wasifu wa kampuni (Company Profile)
- 2) Muombaji **lazima** awe na uwezo wa kupeleka vifaa hadi eneo la ujenzi
- 3) Muombaji atatoa risiti za EFD baada ya kupunguza kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kilichosamehewa.
- 4) Malipo yote yatafanyika kupitia Benki
- 5) Uchambuzi wa maombi utafanyika kulingana na bei halisi ya soko kwa kila kifaa kinachohitajika katika mradi, na siyo ujumla wa vifaa vilivyopo kwenye hati msako (quotation)
- 6) Muombaji atakayeshinda kuleta vifaa vya Ujenzi lazima asaini mkataba/makubaliano kabla ya kuleta vifaa alivyoshinda.
- 7) Hati msako/nukuu za bei (quotation) zinapatikana kwenye ofisi ya mkuu wa shule ya msingi Namkuku kwa kila **LOT** malipo ya kablasha la nukuu ya bei yatafanyika katika ofisi ya Mkurugenzi wa mji. Waombaji wote wapitie ofisi Na. 18 kwa maelekezo
- 8) Inasisitizwa kuwa waombaji lazima wajaze bei ya vifaa vya ujenzi baada ya vifaa hivyo kupokelewa katika eneo la Ujenzi.
- 9) Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono kupitia, **Ofisi ya Mkuu wa shule ya Namkuku kwa Anuani ifuatayo :-**

**MKUU WA SHULE,  
SHULE YA MSINGI NAMKUKU,  
S.L.P 1490,  
NANYAMBA.**

**Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 13.08.2023 saa 04:30 Asubuhi na ndiyo siku ya ufunguzi.**



**Mkuu wa shule  
MWALIMU MKUU  
S/ MSINGI NAMKUKU  
S.L.P 1490 NANYAMBA**